# Ulega akunwa TADB kusaidia sekta ya maziwa

Mwandishi Wetu, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Tabora.** Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega ameipongeza Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa mchango inaoutoa kwenye sekta ndogo ya maziwa nchini.

Waziri Ulega alitoa pongezi hizo alipotembelea banda la benki hiyo katika maonyesho ya wiki ya maziwa yaliyomalizika mwishoni mwa wiki mkoani Tabora.

Alisema Tanzania ni moja kati ya nchi zenye ng'ombe wengi barani Afrika na kusisitiza uwekezaji wa kimkakati katika sekya ya mifugo utasaidia kuongeza uzalishaji katika mnyoro wa thamani na kuboresha maisha ya wafugaji wadogo na nchi kwa ujumla.

"TADB inafanya kazi nzuri katika kusaidia maendeleo ya sekta ya mifugo pamoja na mnyororo wake wa thamani. Hata hivyo, bado kuna fursa nyingi hazijatumika katika sekta ya mifugo na hii inaonyesha kuwa bado kuna kazi kubwa inapaswa kufanyika," alisema.

Alisema wizara imeanzisha mradi wa BBT utakaojikita kwenye mifugo pekee na kuongeza kuwa mradi huo utafanyika Tabora, moja ya mikoa yenye ng'ombe wengi nchini na kuiagiza TADB kuungana na timu kutoka wizarani kutekeleza mradi huo.

Kaimu meneja wa TADB Kanda ya Magharibi, Furaha Sichula alisema benki hiyo kwa kushirikiana na wadau wengine inatekeleza mradi shirikishi wa wasindikaji na wazalishaji wa maziwa (TI3P) unaolenga kuwanufaisha wafugaji wadogo 100,000 wa ng'ombe wa maziwa pamoja na wachakataji.

Sichula alisema mpaka sasa wamewezesha uwekazji wa dola milioni 7.7 za Marekani (Sh bilioni 17 kwenye kuwasidia wasindikaji wadogo na wachakataji wa maziwa hapa nchini.

"Jumla ya wakulima 19,124 na wajasiriamali wadogo na wa kati wamepatiwa mafunzo kwenye eneo la fedha. Pia wameelekezwa fursa za kifedha zilizopo katika sekta, mahitaji na utaratibu wa kupata mikopo kutoka TADB," alisema.



Kiongozi wa ACT Wazalendo, Zitto Kabwe akizungumza na wakazi wa Katoro aliposimama kuwasalimia wakati akielekea Geita mjini kwa ajili ya mkutano wa hadhara wa chama hicho. **Picha na Ericky Boniphace**

# Zitto: Wafugaji sasa watengewe maeneo maalumu

Bakari Kiango na Jesse Mikofu,
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Geita/Ugunja.** Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe ameitaka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kutenga maeneo ya malisho na kunyweshea mifugo ili wafugaji wafanye shughuli zao pasipo mwingiliano na wakulima.

Alisema bado kuna changamoto ya wakulima na wafugaji mkoani Geita akitolea mfano kijiji cha Msasa Tarafa ya Busanda ambapo kila mwaka kunatokea migogoro ya makundi hayo mawili na kusababisha madhara kwa wananchi.

Zitto alitoa kauli hiyo jana wakati akihutubia katika mkutano wa hadhara uliofanyika uwanja wa Namkumbu stendi ya Malori wilayani Geita mkoani hapa, katika mwendelezo wa ziara ya kuimarisha chama.

Katika ziara hiyo, Zitto aliambatana na Mwenyekiti wa chama hicho, Juma Duni Haji na Makamu Mwenyekiti (Bara) Dorothy Semu.

"Wafugaji wa Geita hasa Bukombe hawana malisho, ndiyo maana hujikuta mifugo yao inakamatwa kwenye hifadhi. Pia migogoro ya wakulima na wafugaji inasababisha watu kupoteza maisha.

"Ndiyo maana tunaitaka Serikali iwatengee eneo kubwa la malisho kwa sababu mifugo ina manufaa kwa wafugaji na baadhi yao wana familia na wanasomesha watoto.Haya yakifanyika yatawainua wafugaji na kukuza uchumi wao, pato la Taifa na mtu mmoja mmoja," alisema Zitto.

Mwananchi jana lilimtafuta Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega ambaye alijibu kwa ufupi akisema, "tunayo mipango ndani chama (CCM) na tunayo mipango katika bajeti yetu ya mwaka 2023/24."

Katika bajeti hiyo, iliyowasilishwa mwezi uliopita, Serikali ilisema malisho ni miongoni mwa mambo yatakayopewa kipaumbele kwa kutumia mashamba ya Kampuni za Ranchi za Taifa (Narco) kwa ajili ya uwekezaji wa malisho, unenepeshaji na kupata nyasi.

## Katiba mpya

Katika mkutano wake wa jana, Zitto aligusia suala la Katiba mpya akisema ACT- Wazalendo inataka kabla ya mwisho wa mwaka huu, masuala mbalimbali yatekelezwe ikiwemo Sheria ya mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2011 kuhuishwa kwa kuweka utaratibu mpya wa kukamilisha mchakato wa Katiba.

"Kuwepo kwa mkutano wa Kitaifa wa kupata mwafaka wa masuala maalumu kama vile muundo wa Muungano, kuundwa kwa timu ya wataalamu ili kuandika rasimu mpya ya Katiba na kura ya maoni ya Katiba mpya.

Waziri Kivuli wa Fedha na Mipango wa ACT- Wazalendo, Immanuel Mvula aliitaka Serikali kutazama upya sheria ya madini na sera zake ili rasilimali hiyo ya kimkakati iache athari chanya zaidi Tanzania hasa kwa wakazi wa maeneo husika sio mashimo tu.

"Tunataka ijengwe miji ya madini karibu na maeneo ya uchimbaji ili kuongeza mzunguko wa kiuchumi na kukuza miji," alisema Mvula ambaye ni mjumbe wa kamati kuu ya chama hicho.

## Walia na Dk Mwinyi

Katika hatua nyingine, chama hicho kimesema licha ya Rais wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi kutetea Serikali yake kukiuka sheria ya manunuzi kwa misingi ya dharura lakini sababu alizotaja hazipo kwenye sheria hiyo.

Kauli hiyo imetolewa jana na Mjumbe wa Kamati Kuu ya chama hicho, Ismail Jussa wakati wa mkutano wa hadhara wa chama hicho uliofanyika

> **"Kutungwa kwa Sheria mpya ya Uchaguzi ili kuwa na Tume Huru ya Uchaguzi, sambamba na Sheria mpya ya Vyama vya Siasa, tutoke kwenye maneno twende kwenye vitendo.Tutoke kususasusa twende kwenye mjadala ili kupata Katiba mpya na Tume Huru ya Uchaguzi."**
>
> Zitto Kabwe

Nyarugusu Zanzibar.

Kutokana ukiukwaji wa sheria unaofanywa, Jussa alisema hakuna mwekezaji atakwenda Zanzibar kuwekeza fedha zake.

Alisema utaratibu ndio msingi wa kila kitu hivyo watafichua hayo na kuhakikisha mwaka 2025 wanafungashia vilago Serikali iliyopo na huo ndio utakuwa mwisho wa ukiukwaji wa Utawala wa sheria.

Jussa alisema kwa mujibu wa sheria ya manunuzi vifungu vya 67, 71 na 73 vinaeleza wazi kwamba masuala ya dharura ni pamoja na maafa, vita na uhamishaji wa mali za umma.

"Sasa jiulize hayo alivyosema yamo kwenye udharura huo? alihoji Jussa huku wanachama na wafuasi wa chama hicho wakisema hakunaaa

Hivi karibuni Dk Mwinyi alisema katika kauli zinazotolewa na chama hicho kwamba Serikali yake inakiuka sheria kujenga miradi bila kufuata utaratibu ikiwemo ujenzi wa uwanja wa Amani na uendeshaji wa bandari ya Malindi ni kutokana na udharura

Katika dharura alizotaja Rais Mwinyi kuhusu Uwanja wa Amani alisema ni kutokana na kuwapo sherehe kubwa za miaka 60 ya Mapinduzi hivyo kungefuatwa utaratibu wa zabuni za wazi ingechelewa

Alisema sheria ya manunuzi ina maeneo matatu ambayo ni zabuni za wazi, mtu mmoja na kushindanisha kampuni mbili iwapo kuna dharura.

Kuhusu dharura ya bandari ya Malindi Dk Mwinyi alisema wameingia mkataba na kampuni ya kigeni kutokana na bandari hiyo kuzidiwa.

Jussa alisema hawatakubali kuendelea kwa vitendo hivyo na kujificha kwenye kivuli cha dharura kwasababu kupitia njia hiyo kunafanyika ubadhirifu kama ilivyoeleza ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

CamScanner